

Kuzuia Kuenea kwa VVU – Mama-hadi-Mtoto

Kuenea kwa VVU kutoka kwa mama-hadi-mtoto ni njia ya kawaida sana ambayo watoto wanaambukizwa VVU. Watoto wadogo ambao wako na VVU huenda waliambukizwa:



- Wakati wa ujauzito wa mama
- Wakati wa kuzaa mtoto kupitia kwa uke
- Kwa kunywa maziwa yaliyoambukizwa kutoka kwa mama yao aliye na VVU

Kuna matibabu yanayoweza kumlinda mtoto kutokana na kupata VVU. Wakati mama wa VVU wanapokea madawa ambayo yanapigana na virusi vya VVU wakati wa ujauzito, na kujifungua wanapata watoto kwa *kupitia njia ya kupasuliwa* (Mfumo wa C), kiwango cha kupata VVU kwa watoto wao hushuka hadi asilimia 2. Watoto waliozaliwa na wamama walio na VVU pia hupewa madawa ya VVU (antiretrovirals) wakati wa kuzaliwa.



Pia kuna matibabu saidizi ya wanawake ambao hawawezi kujua kuwa wana VVU hadi hadi wawe katika hali ya

kujifungua. Wakati wanapokea matibabu ya VVU wakati wa kusikia uchungu na kujifungua, hatari ya maambukizi ya VVU kwa watoto wao inaweza kupungua hadi chini ya asilimia 10%. Mama aliye na VVU

ambaye hatumii madawa ya VVU (antiretrovirals) wakati wa ujauzito, uchungu au kujifungua ana nafasi hadi asilimia 25 ya kueneza virusi kwa mtoto wake.

Kama unataka kujifungua kwa njia ya upasuaji au njia ya uke ni jambo ambalo unafaa kujadiliana na mtoaji huduma ya afya wako wakati wa ujauzito wako. Itategemea na afya yako, hali ya tiba ya VVU, na jinsi hali yako ya uchungu inaendelea wakati wa kujifungua.

Kupimwa kwa VVU kwa Wanawake Wajawazito



CDC inapendekeza kuwa wanawake wote wajawazito lazima wapimwe VVU-

–lakini si watoaji wote wa huduma ya afya ambao hupima VVU kwa wanawake wajawazito. Kama wewe ni mja mzito na unafikiri kuwa huenda ukawa na VVU au magonjwa ya zinaa (STD), ni bora kuuliza kupimwa VVU.



Watoto Waliozaliwa Kupimwa VVU

Kingamwili ni vitu ambavyo vimeundwa na mwili kupigana na maambukizi. Kupimwa kwa kawaida kwenye mahabara ambako kunaonyesha kama mtu ameambukizwa na VVU hutafuta kingamwili za VVU.

Watoto wote walio zaliwa na wamama walio na VVU wana kingamwili kwa VVU. Kingamwili hizi ziliundwa na mfumo wa kingamaradhi ya mama na huingia kwa mkondo wa damu ya mtoto kabla ya kuzaliwa. Kingamwili hizi zinaweza kuwa hadi miezi 18. Kingamwili hizi zinaonyesha kuwa mama alikuwa ameambukizwa VVU, lakini haimanishi kuwa mtoto ameambukizwa.



Hakikisha kupata majibu ya maswali yoyote unayo kuhusu VVU/UKIMWI. Idaro yako ya afya ya umma na mtoaji matunzo ya afya wanaweza kusaidia.

Hii inamaanisha kuwa jaribio wastani ya kipimo cha kingamwili ya maambukizo ya VVU si muhimu kwa watoto wadogo au watoto wachanga. Watoaji huduma ya afya hutumia jaribio maalum ya VVU ambazo zinaweza kutambua viwango kidogo vya virusi wenyewe katika damu ya watoto ambao wako chini ya umri wa



miezi 6. (Kumbuka, jaribio nyingi ya VVU huangalia kingamwili kwa virusi, si virusi pekee.) Kwa jaribio maalum, madaktari wanaweza kutambua karibu asilimia 90 ya watoto walioambukizwa VVU wakati wako na umri wa miezi 2, na asilimia 95% wakati wako na umri wa miezi 3. Watoto wote waliozaliwa na wamama walio na VVU wanafaa kupimwa VVU kila mara wakati wa mwaka wa kwanza.

Kama wewe una VVU na mjamzito, ni muhimu kuzungumza na mtoaji wako wa huduma ya afya kuhusu mipango ya matibabu yako na ya mtoto wako baada ya kujifungua.

Text adapted from materials on the AIDS.gov website.
Handout by Healthy Roads Media (www.healthyroadsmedia.org),
Funding from Division of Specialized Information Services of the
National Library of Medicine. It can be freely distributed under the
Creative Commons Attribution-NonCommercial-NoDerivs License
(<http://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/3.0/us>)

Swahili

HIV/AIDS – Pregnancy and Childbirth
Last reviewed 2013